

CHAMA CHA WAFANYAKAZI
SERIKALI ZA MITAA TANZANIA

TANZANIA LOCAL GOVERNMENT
WORKERS UNION
(TALGWU)

KATIBA YA CHAMA
TOLEO LA 2016

CHAMA KIMESAJILIWA CHINI YA SHERIA YA
AJIRA NA MAHUSIANO KAZINI
(THE EMPLOYMENT AND LABOUR RELATION ACT)
NA. 6 YA 2004

Toleo hili la Katiba ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) la mwaka 2016 ni toleo la sita tangu Katiba hii itungwe mwaka 1995

Toleo hili limezingatia na kuweka pamoja marekebisho yaliyofanywa katika Katiba ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Matoleo ya 1995,1999, 2001, 2006 na 2011

KATIBA YA CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA

AZIMIO LA MKUTANO WA KWANZA WA TALGWU TAIFA

Kwa kuwa sisi Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania tuliokutana hapa Dodoma tarehe Ishirini (20) na Ishirini na Moja (21) Aprili, mwaka Elfu Moja Mia Tisa Tisini na Tano (1995) kwa niaba ya Wafanyakazi wote wa Serikali za Mitaa, zikiwemo Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji, Halmashauri za Wilaya na Mashirika ya Uchumi Nchini. Sisi sote kwa pamoja tumeamua kupitisha KATIBA YA CHAMA kwa dhati, kuzingatia misingi ya haki, uhuru, udugu na mshikamano;

Kwa kuwa sisi Wawakilishi wa Wafanyakazi tunathibitisha msimamo wetu kuthamini heshima ya kazi, misingi ya demokrasia, kukuza usawa kwa wote, kupiga vita aina zote za ubaguzi au uonevu na unyanyasaji wa jinsia, utaifa, ukabila, udini au mahali mtu anapotoka;

Kwa kuwa sisi wawakilishi wa Wafanyakazi tunatambua kuwa umaskini popote pale unasababisha umaskini mahala pengine;

Kwa kuwa sisi Wawakilishi wa Wafanyakazi tunatambua Mshikamano miongoni mwa Vyama vya Wafanyakazi unatokana na kuelewa kwamba matatizo ya wafanyakazi yana mtazamo unaofanana, unaodhihirishwa na kushauriana kwetu kwa kila mara;

Kwa sababu hiyo basi, Katiba hii ya Chama inakubaliwa na kupitishwa kwa ajili ya utekelezaji wa nia na madhumuni yaliyotajwa.

YALIYOMO

AZIMIO LA MKUTANO WA KWANZA WA TALGWU TAIFA

SURA YA KWANZA

JINA, TAFSIRI, IMANI, MADHUMUNI NA KUJISHIRIKISHA

1.1 Jina la Chama 1
1.1.1 Makao Makuu ya Chama 1
1.2 **Tafsiri** **1**
1.2.1 Chama **1**
1.2.2 Mwajiri 1
1.2.3 Mfanyakazi 2
1.2.4 Mwanachama 2
1.2.5 Uanachama wa Heshima 2
1.2.6 Kiongozi 2
1.2.7 Katibu Mkuu 2
1.2.8 Afisa wa Chama 2
1.2.9 Sekretarieti 3
1.2.10 Kijana 3
1.2.11 Makubaliano ya Mkataba 3
1.2.12 Mgogoro 3
1.2.13 Mgomo 3
1.2.14 TUCTA 3
1.2.15 Mkoa 3
1.2.16 Wilaya 4
1.2.17 Tawi 4
1.2.18 Kamati ya Tawi 4
1.2.19 Bendera ya Chama 4
1.3 **Imani ya Chama** 4

1.4 Madhumuni ya Chama 5

1.5 Kujishirikisha 6

1.5.1 Uhusiano wa Kimataifa 7

SURA YA PILI

UANACHAMA NA MICHANGO

2.1 Usajili wa Wanachama. 8

2.2 Orodha ya Wanachama 8

2.3 Sifa za Mwanachama 8

2.4 Haki za Mwanachama 9

2.5 Wajibu wa Mwanachama 10

2.6 Ukomo wa Uanachama 10

2.7 Kujitoa katika Chama 10

2.8 Kuachishwa Uanachama 11

2.9A Utaratibu wa kuachisha au kusimamisha Mwanachama 11

2.9B Haki ya kukata Rufaa 12

2.10 Kuhama kwa Mwanachama kutoka sehemu ya Kazi kwenda sehemu nyingine ya Kazi.....12

2.11 Kufutwa katika Orodha ya Wanachama 12

2.12 Haki ya Kujihushisha na Shughuli za chama 13

2.13 Uanachama wa Heshima 13

2.14 Michango ya Wanachama 13

2.14.1 Michango ya kila mwezi 13

2.14.2 Michango Maalum 14

2.14.3 Ada ya Uwakala 14

SURA YA TATU

AJIRA NA UWAKILISHI

3.1 Sehemu ya Ajira na Uwakilishi 15

3.2 Idara za Huduma katika Chama.....15

3.3 Uanzishaji na Ubadilishaji wa Idara na Vitengo 16

SURA YA NNE

VIONGOZI WA CHAMA

4.1 Uchaguzi na Viongozi 17

4.2 Ukomo wa Uongozi 17

4.3 Utaratibu wa kusimamishwa Uongozi 18

4.4 Ukomo wa vipindi vya Uongozi 18

4.5 Muda wa Kujaza nafasi zilizo wazi 19

SURA YA TANO

VIKAO VYA CHAMA

5.1 Ngazi za Vikao vya Chama 20

5.2 Vikao vya Tawi 20

5.3 Mkutano wa Wanachama wote 21

5.3.1 Wajumbe wa Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi 21

5.3.2 Kazi za Mkutano wa Wanachama wote 22

5.4 Mkutano wa Wafanyakazi wote wa Tawi 23

5.4.1 Wajumbe wa Mkutano wa Wafanyakazi wote 23

5.4.2 Kazi za Mkutano za Wafanyakazi wote 23

5.5 Halmashauri Kuu ya Tawi 24

5.5.1 Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi 24

5.5.2 Kazi za Halmashauri Kuu ya Tawi 25

5.6 Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi 26

5.6.1 Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi 26

5.6.2 Kazi za Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi 27

5.7 Viongozi wa Chama katika Tawi 28

5.7.1 Mwenyekiti wa Tawi 28

5.7.2 Kazi za Mwenyekiti wa Tawi 29

5.7.3 Katibu wa Tawi 29

5.7.4 Kazi za Katibu wa Tawi 29

5.8 Vikao vya Chama katika Halmashauri 30

5.8.1 Kamati ya Uratibu 30

5.8.2 Wajumbe wa Kamati ya Uratibu 30

5.8.3 Kazi za Kamati ya Uratibu 30
5.9 Vikao vya Chama katika Mkoa 31
5.10 Mkutano Mkuu wa Mkoa 31
5.10.1 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa 32
5.10.2 Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa 33
5.11 Kamati ya Utendaji ya Mkoa 34
5.11.1 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa 35
5.12 Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa 36
5.12.1 Wajumbe wa Kamati ya Ushaurin ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa 36
5.12.2 Kazi za Kamati yta Ushauri Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa 36
5.13 Viongozi wa Chama wa Mkoa 38
5.13.1 Mwenyekiti wa Mkoa 38
5.13.2 Kazi za Mwenyekiti wa Mkoa 38
5.13.3 Katibu wa Mkoa 39
5.13.4 Kazi za Katibu wa Mkoa 39
5.14 Vikao vya Talgwu Taifa 40
5.15.1 Mkutano Mkuu wa Taifa 40
5.15.2 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa 41
5.15.3 Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa 42
5.16.1 Baraza Kuu la Taifa 43
5.16.2 Wajumbe wa Baraza Kuu 43
5.16.3 Kazi za Baraza Kuu la Taifa 44
5.17.1 Kamati ya Utendaji ya Taifa 46
5.17.2 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa 46
5.17.3 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Taifa 47
5.18.1 Kamati ya Ushauri ya Wafanykazi wanawake ya Taifa 48
5.18.2 Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Taifa Ukurasa 48
5.18.3 Kazi za Kamati ya Ushauri ya WSafanyakazi Wanawake ya Taifa 49
5.19 Viongozi wa Chama Taifa 51
5.19.1 Mwenyekiti wa Chama Taifa 51
5.19.2 Makamu Mwenyekiti wa Taifa 52

5.19.3 Katibu Mkuu wa Chama Taifa 52ssss

5.19.4 Kazi za Katibu Mkuu wa Chama 52

5.19.5 Naibu Katibu Mkuu wa Chama 53

5.19.6 Mweka Hazina wa Chama Taifa 54

SURA YA SITA

WADHAMINI WA CHAMA

6.0 Wadhamini wa Chama 55

6.1 Vikao vya Wadhamini 55

6.2 Sifa za Wadhamini 55

6.3 Kazi na wajibu wa Wadhamini 55

6.4 Ukomo wa Wadhamini 56

SURA YA SABA

MALI, VITEGA UCHUMI NA MIKOPO YA CHAMA

7.0 Mali Vitega Uchumi na Mikopo ya Chama 57

SURA YA NANE

8.1 Uwasilishaji wa Hoja 58

8.2 Mapato ya Chama 59

8.3 Mgawanyo wa Mapto ya Chama 59

8.4 Ukaguzi wa Fedha za Chama 59

8.5 Utata wa Tafsiri ya Katiba 59

8.6 Kuvunjika kwa Chama au kuunganisha Vyama 60

8.7 Upigaji wa Kura 60

8.8 Migogoro ya Kikazi au Mijadala na Mwenendo 61

SURA YA KWANZA

JINA, TAFSIRI, IMANI, MADHUMUNI NA KUJISHIRIKISHA

1.1 JINA LA CHAMA

Jina la Chama litakuwa TANZANIA LOCAL GOVERNMENT WORKERS UNION kwa kifupi (TALGWU) au Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania.

1.1.1 Makao Makuu ya Chama

Makao Makuu ya Chama yatakuwa Dar es Salaam na anuani yake itakuwa S.L.P. 16097 – DAR ES SALAAM.

1.2 TAFSIRI

Katika Katiba hii, kama haikuelezwa vinginevyo na Sheria yoyote ya nchi, maneno yaliyoainishwa katika Ibara hii yatakua na maana ifuatayo;

1.2.1 “Chama”

Ni Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU).

1.2.2 “Mwajiri”

Ni Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika huru yanayotekeleza majukumu ya Serikali za Mitaa, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, Mfuko wa Pensheni wa LAPF, na Mamlaka nyingine za Ajira.

1.2.3 “Mfanyakazi”

Ni mtu aliyeingia katika Makubaliano au Mkataba na Mwajiri yoyote yule kwa kupewa malipo ya Ujira au Mishahara.

1.2.4 “Mwanachama”

Ni mfanyakazi yoyote aliyeajiriwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Mashirika huru yanayotekeleza majukumu ya Serikali za Mitaa na Mamlaka nyingine za Ajira na aliyesajiliwa na Chama.

1.2.5 “Uanachama wa Heshima”

Uanachama wa Heshima unaweza kutunukiwa kwa Wanachama au Waasisi waliojitolea wakati wa enzi zao katika kukiendeleza Chama, au kwa mtu yoyote ambaye Chama kitaona anafaa.

1.2.6 “Kiongozi”

Ni mwanachama yoyote aliyechaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

1.2.7 “Katibu Mkuu”

Ni Mtendaji Mkuu wa Chama au Afisa wa Chama aliyeidhinishwa kutenda shughuli za Chama kwa niaba yake.

1.2.8 “Afisa wa Chama”

Ni mtu yoyote aliyeajiriwa na Chama katika kada za manejimenti za Chama kwa Mkataba wa Kudumu.

1.2.9 “Sekretarieti”

Ina maana ya Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara na Vitengo vilivyo chini yake.

1.2.10 “Kijana”

Ni mtu mwenye umri wa miaka kumi na nane hadi thelathini na tano

1.2.11 “Makubaliano ya Mkataba”

Ni maelewano yaliyofikiwa kati ya Mwajiri na Mwanachama, Wanachama au Chama chake kwa niaba ya Mwanachama au Wanachama

1.2.12 “Mgogoro”

Ni kuwepo kwa hali isiyokuwa na maelewano kati ya Mwajiri na Mfanyakazi na Wanafanyakazi wake kwa ujumla yanayohusu masuala ya kazi.

1.2.13 “Mgomo”

Ina maana ya uamuzi wa wafanyakazi kusimamisha shughuli zinazoendeshwa na Mwajiri kwa mujibu wa Sheria za nchi.

1.2.14 “TUCTA”

Ni kifupi cha Trade Union Congress of Tanzania au Shirikisho la Vyama vya Wafanyazi Tanzania ambalo Chama hiki kimejishirikisha.

1.2.15 “Mkoa”

Ni eneo litakalotangazwa rasmi na Baraza Kuu la Chama kuwa na hadhi ya Mkoa.

1.2.16 "Wilaya"

Ni eneo la Halmashauri litakalotangazwa rasmi na Baraza Kuu la Chama kuwa na hadhi ya Wilaya.

1.2.17 "Tawi"

Ni muunganiko wa wanachama kumi au zaidi walioajiriwa mahala pa kazi.

1.2.18 "Kamati ya Tawi"

Ni Halmashauri ya Tawi mahala pa kazi.

1.2.19 "Bendera ya Chama"

Kutakuwa na bendera ya Chama ambayo itakuwa na alama zifuatazo;

(i) Rangi ya kijani angavu (Light Green)

(ii) Nembo ya TALGWU katikati na maneno ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU).

1.3 IMANI YA CHAMA.

Chama kinaamini kuwa:

1.3.1 Wafanyakazi wote duniani ni sawa

1.3.2 Kila mfanyakazi ana haki ya kufanya kazi na anastahili malipo kufuatana na kazi yake pamoja na kuheshimiwa kama binadamu.

1.3.3 Mshikamano wa wafanyakazi wote Duniani daima ndiyo njia pekee itakayokuza ushirikiano wa karibu kati ya wafanyakazi na Vyama vyao katika nchi zote.

1.3.4 Nguvu ya wafanyakazi itatokana na juhudi zao katika kukuza umoja.

1.3.5 Utengano wa aina yoyote kati ya wafanyakazi ni alama ya udhaifu.

1.3.6 Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) hakitakuwa Mwanachama au kuwa na mahusiano yoyote ya Kikatiba na chama chochote cha siasa ila wanachama wa TALGWU watakuwa huru kujiunga na Chama chochote cha siasa.

1.3.7 Ili kuepuka migogoro na migongano ya kimaslahi, wafanyakazi wa Chama wenye mikataba ya kudumu hawataruhusiwa kushika nafasi za uongozi katika vyama vya siasa.

1.4 MADHUMUNI YA CHAMA

Chama hiki si kwa ajili ya kipato, na madhumuni yake yatakuwa yafuatayo;

1.4.1 Kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya wanachama katika maisha yao wakiwa kazini.

1.4.2 Kupigania na kuwahimiza waajiri kuboresha na kuendeleza hali ya wanachama katika maisha yao wakiwa kazini na wakati wa kustaafu.

1.4.3 Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya Mwajiri na Mwanachama, au Mwanachama mmoja na mwengine kwa njia ya makubaliano ya amani kila itakapowezekana.

1.4.4 Kusaidia uandaaji wa utekelezaji wa Mikataba ya Hiari na Tuzo.

1.4.5 Kuwaelimisha wanachama kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Nidhamu zinazotumika nchini.

1.4.6 Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na vyama vingine vya wafanyakazi nchini pamoja na vile vya kimataifa kwa lengo la kuboresha maslahi ya wanachama wake.

1.4.7 Kufanya tafiti na kuishauri Serikali kuhusu sera nzuri za kuendeleza Uchumi kwa maslahi ya wanachama na maisha ya jamii kwa ujumla.

1.4.8 Kulinda maslahi ya wanachama kwa kuwasiliana na Serikali ili kuepukana na uandaaji wa Sera na Sheria ambazo ni hatari kwa wanachama.

1.4.9 Kuwahimiza wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii na uadilifu wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

1.5 KUJISHIRIKISHA

Chama kitajishirikisha na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini, (TUCTA) au Shirikisho jingine kama ambavyo Chama kitaona inafaa, na kitawakilisha wanachama wote wanaotokana na ajira ya Serikali za Mitaa na wale wanaotokana na mamlaka nyingine za ajira.

1.5.1 Uhusiano wa Kimataifa

Chama kinaweza kuwa na uhusiano wa vyama vingine vya sekta ya Serikali za Mitaa ambavyo vinajumuisha Jiji, Manispaa, Halmashauri za Miji, Wilaya na Vitengo vyake vya Uchumi katika Nchi mbalimbali, na kujiunga na Muungano wa wafanyakazi wa Kimataifa kila inapohitajika kufanya hivyo kwa maslahi ya chama.

SURA YA PILI

UANACHAMA NA MICHANGO

2.1 Usajili wa Wanachama

Usajili wa wanachama utafanywa kwa kila mwanachama kujaza fomu maalum ya usajili (TUF 6) ambayo itakuwa na maelezo ya Mwanachama pamoja na maelekezo yake kwa mwajiri ya kukata ada ya uanachama na kuiwasilisha kwa Chama.

2.2 Orodha ya Wanachama

Baada ya kusajiliwa na Chama maelezo ya mwanachama yaliyomo katika Kadi ya Uanachama yataingizwa katika Orodha ya Wanachama (TUF 15) kwa madhumuni ya kusaidia kuweka kumbukumbu za michango ya wanachama na kumbukumbu hizo zitatakiwa kwa sahihi kila wakati.

2.3 Sifa za Mwanachama.

Mwanachama wa TALGWU atatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;

(i) Awe ni mfanyakazi yoyote aliyeajiriwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Mashirika huru yanayotekeleza majukumu ya Serikali za Mitaa na Mamlaka nyingine za Ajira.

(ii) Awe amesajiliwa na Chama kwa mujibu wa Sheria

(iii) Awe analipa michango yake ya kila mwezi isipokuwa kwa wanachama wa heshima

(iv) Awe tayari kusaidia Chama kwa vitendo katika utekelezaji madhumuni yake kwa ujumla.

(v) Awe muaminifu, muadilifu, mzalendo na mtii kwa Chama na asimamie utekelezaji wa Katiba na Kanuni za Chama.

2.4 Haki za Mwanachama

Mwanachama yoyote isipokuwa mwanachama wa heshima, atakuwa na haki zifuatazo:

2.4.1 Kuwakilishwa na Chama dhidi ya mwajiri wake pamoja na haki ya yeye mwenyewe kujitetea dhidi ya mwajiri huyo kwa mashtaka yoyote dhidi yake.

2.4.2 Kujitetea mbele ya vyombo mbalimbali vya Chama na hali ya kukata rufaa katika vyombo vya juu vya Chama pale ambapo itabidi, kama hataridhika na uamuzi uliotolewa.

2.4.3 Haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

2.4.4 Haki ya kuweza kufahamu hesabu ya mali na fedha za Chama.

2.4.5 Ili kuepuka migongano ya kimaslahi, wanachama waajiriwa wa Chama hawataruhusiwa kupiga kura katika chaguzi za viongozi wa Chama au kugombea nafasi za uongozi wa Chama zisizo za kiutendaji.

2.5 Wajibu wa Mwanachama.

Kila Mwanachama atakuwa na wajibu wa:

2.5.1 Kulipa michango ya kila mwezi na malipo maalumu kwa wakati unaotakiwa.

2.5.2 Kuunga mkono na kusaidia kwa vitendo maendeleo ya Chama.

2.5.3 Kuzingatia Kanuni na taratibu za Chama na kuheshimu maamuzi yaliyotokana na kanuni na taratibu hizo.

2.5.4 Kuhudhuria vikao vya Chama kwa mujibu wa Katiba.

2.6 Ukomo wa Uanachama

Uanachama utakoma kwa mojawapo wa sababu zifuatazo;

2.6.1 Kutolipa michango kwa miezi sita (6) mfululizo.

2.6.2 Kujitoa katika Chama

2.6.3 Kuacha au kuachishwa kazi

2.6.4 Kustaafu kwa mujibu wa sheria za nchi.

2.6.5 Kuvuliwa uanachama

2.6.6 Kufariki

2.7 Kujitoa katika Chama

Mwanachama anaweza kujiuzulu uanachama wake kwa kumuandikia Katibu Mkuu wa Chama kupitia Kamati ya Utendaji Mkoa au Halmashauri ya Tawi lake, na kutoa notisi ya siku thelathini kwa mujibu wa Sheria za nchi.

2.8 Kuachishwa Uanachama.

Mwanachama yoyote awe Afisa wa kuchaguliwa au kuteuliwa anaweza kuachishwa uanachama kama:

2.8.1 Atagundulika kuwa alijipatia uanachama kwa njia ya udanganyifu.

2.8.2 Kwa kukosa uaminifu, kufuja au kupoteza mali za Chama.

2.8.3 Amegundulika kuwa vilevile ni mwanachama wa Chama kingine kinachoshindana na Chama hiki.

2.8.4 Atafanya vitendo vinavyopingana na Kanuni, Maadili ya Chama au uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Chama.

2.8.5 Amekosa uzalendo na utii kwa Chama kwa mfano kujihusisha na masuala ya kukisaliti Chama katika migogoro ya kikazi au kutoa siri za Chama.

2.9A Utaratibu wa kuachisha au kusimamisha Mwanachama

Utaratibu wa kuachisha au kusimamisha mwanachama utakuwa kama ifuatavyo:

a) Halmashauri a Tawi itatoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Uratibu ya Halmashauri.

b) Kamati ya Uratibu ya Halmshauri itatoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Utendaji Mkoa.

c) Kamati ya Utendaji Mkoa baada ya kuchunguza mapendekezo ya Kamati ya Uratibu ya Halmashauri nayo itatoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

d) Kamati ya Utendaji Taifa baada ya kufanyia kazi mapendekezo ya Kamati ya Utendaji Mkoa, itatoa uamuzi kama itakavyoona inafaa.

2.9B Haki ya Kukata Rufaa

Mwanachama aliyeachishwa uanachama na Kamati ya Utendaji ya Taifa atakuwa na haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa Baraza Kuu Taifa ndani ya kipindi cha siku tisini tangu uamuzi wa kuachishwa unapotolewa

2.10 Kuhama kwa Mwanachama kutoka sehemu moja ya kazi kwenda sehemu nyingine ya kazi.

Mwanachama anayehama sehemu moja ya kazi kwenda sehemu nyingine atatoa taarifa katika Tawi la karibu la mahala pengine pa kazi na kuendelea kuwa Mwanachama wa Chama hiki.

2.11 Kufutwa katika orodha ya Wanachama.

Mwanachama ambaye uanachama wake utakoma kwa sababu yoyote ile, jina lake litafutwa katika orodha ya wanachama na atatakiwa kurudisha kadi ya Uanachama.

2.12 Haki ya Kujihusisha na Shughuli za Chama

Mtu yoyote ambaye uanachama wake utakoma katika Chama kwa sababu yoyote ile hatakuwa na haki ya kujihusisha na mali za Chama.

2.13 Uanachama wa Heshima

Uanachama wa Heshima unaweza kutunukiwa kwa Wanachama au Waasisi waliojitolea wakati wa enzi zao katika kukiendeleza Chama, au kwa mtu yoyote ambaye Chama kitaona inafaa.

2.13.1 Uanachama wa Heshima unaweza kutunukiwa kwa Wanachama au Waasisi waliojitolea wakati wa enzi zao katika kukiendeleza Chama, au kwa mtu yoyote ambaye Chama kitaona inafaa.

2.13.2 Uchaguzi au uteuzi wa wanachama wa Heshima utafanywa na Mkutano Mkuu wa Chama Taifa.

2.13.3 Wanachama wa Heshima hawataruhusiwa kupiga kura katika Mikutano ya Chama.

2.13.4 Mwanachama wa Heshima atakuwa na majukumu kama yatakayoainishwa kwenye Kanuni za Chama.

2.14 MICHANGO YA WANACHAMA

2.14.1 Michango ya kila mwezi.

Kila mwanachama atalipa mchango wa asilimia mbili (2%) ya mshahara wake wa kila mwezi. Michango ya kila mwezi italipwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Michango inaweza kulipwa na mwanachama kwa kupeleka moja kwa moja Tawini kwake na akapewa stakabadhi.

b) Kwa kukatwa na mwajiri kwa njia ya “Lawson System” Michango inapopokelewa na Chama, mwajiri atapewa stakabadhi ya michango hiyo iliyopokelewa.

c) Malipo yote yatakayofanywa na wanachama yatapelekwa Benki katika akaunti iliyofunguliwa na Chama kama itakavyoelekezwa na Katibu Mkuu wa Chama.

2.14.2 Michango maalum.

Kila watakapotakiwa, wanachama watawajibika kutoa michango maalum itakayopendekewa na Kamati ya Utendaji Taifa na kuamuliwa na Baraza Kuu katika masuala yanayohusiana na migomo na matatizo mengine mahala pa kazi

2.14.3 Ada ya Uwakala

Mahali popote pa kazi ambapo wanachama watazidi asilimia hamsini ya wafanyakazi wote walioajiriwa, Mwajiri atalazimika kukata 2% ya fedha kama ada ya uwakala ya Chama kutoka katika mishahara ya wafanyakazi wasiokuwa wanachama wa TALGWU na wasio wanachama wa Chama kingine cha wafanyakazi mahali hapo pa kazi, na kupeleka fedha hizo katika akaunti ya Chama iliyoko Benki kama itakavyoelekezwa na Katibu Mkuu wa Chama na makato hayo yatafanyika kwa mujibu wa sheria.

SURA YA TATU

AJIRA NA UWAKILISHI

3.1 Sehemu za Ajira na Uwakilishi

Zifuatazo zitakuwa ndizo sehemu za ajira zinazowakilishwa katika Chama hiki:

(i) Halmashauri za Majiji na Idara zake.
(ii) Halmashauri za Manispaa na Idara zake
(iii) Halmashauri za Miji na Idara zake
(iv) Halmashauri za Wilaya na Idara zake
(v) Mashirika ya Uchumi ya Halmashauri
(vi) Chama cha Wafanyakzi wa Serikali za Mitaa (TALGWU)
(vii) Mfuko wa Pensheni wa LAPF
(viii) Mamlaka nyingine za Ajira.

3.2 Idara za Huduma katika Chama

Kutakuwa na Idara za Huduma zifuatazo:

(i) Elimu, Jinsia na Uimarishaji
(ii) Habari na Uhusiano wa Kimataifa
(iii) Fedha
(iv) Utawala na Utumishi
(v) Sheria na Usalama Kazini

3.3 Uanzishaji na ubadilishaji wa Idara na Vitengo

Chama kinaweza kuanzisha Idara nyingine, kitengo au kubadili zilizopo kwa mapendekezo ya Kamati Utendaji Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu.

SURA YA NNE

VIONGOZI WA CHAMA

4.1 Uchaguzi wa Viongozi

4.1.1 Mwanachama anayeomba nafasi ya uongozi wa ngazi yoyote katika Chama atatakiwa awe na vigezo vilivyoainishwa katika Kanuni za Uchaguzi za Chama.

4.1.2 Mgombea wa nafasi yoyote ya uongozi atachaguliwa ikiwa atapata zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa, isipokuwa katika uchaguzi wa kujaza nafasi zaidi ya moja ushindi utahesabiwa kwa kufata wingi wa kura alizopata mwombaji katika nafasi hiyo, bila kujali kama kura hizo zinafikia nusu ya kura zote zilizopigwa.

4.2 Ukomo wa Uongozi.

Uongozi wa Kiongozi utakoma kwa mojawapo ya sababu zifuatazo:

(i) Kujiuzulu
(ii) Kuacha au kuachishwa Uongozi kwa mujibu wa Katiba
(iii) Kujiunga na Chama kingine chochote cha wafanyakazi.
(iv) Kushindwa kutimiza wajibu wake kama kiongozi

(v) Kukoma kwa kipindi cha uongozi

(vi) Kustaafu kwa mujibu wa Sheria za Nchi

(vii) Kusimamishwa uanachama na chombo kinachohusika

(viii) Kuhama eneo husika la uongozi

(ix) Kufariki

4.3 Utaratibu wa Kusimamishwa Uongozi.

(i) Kiongozi aliyechaguliwa uongozi na Mkutano Mkuu wa Taifa atasimamishwa uongozi na Baraza Kuu la Taifa

(ii) Kiongozi aliyechaguliwa na Baraza Kuu atasimamishwa uongozi na Kamati ya Utendaji Taifa

(iii) Kiongozi aliyeteuliwa na Kamati ya Utendaji Taifa atasimamishwa uongozi na Katibu Mkuu wa Chama.

4.3.1 Kiongozi aliyeachishwa uongozi anaweza kuomba tena nafasi ya uongozi wowote katika Chama na maombi yake yatafikiriwa na kutolewa uamuzi na kikao kilichomwachisha uongozi baada ya miaka mitano tangu alipoachishwa uongozi.

4.4 Ukomo wa Vipindi vya Uongozi

Mwanachama yoyote hataruhusiwa kugombea nafasi ya uongozi endapo atakuwa ameshatumikia ngazi hiyo ya uongozi kwa vipindi viwili vya miaka mitano.

4.5 Muda wa kujaza nafasi zilizo wazi

4.5.1 Endapo kiongozi wa Kitaifa ataondoka madarakani kwa sababu yoyote ile, uchaguzi ufanyike ndani ya siku tisini (90) isipokuwa kama ikiwa umebaki mwaka mmoja yaani miezi kumi na mbili (12) kufanyika uchaguzi mkuu nafasi hiyo itakuwa wazi hadi muda wa uchaguzi utakapofika.

4.5.2 Kiongozi wa ngazi yoyote isiyokuwa ya kitaifa akiondoka madarakani kwa sababu yoyote ile, uchaguzi ufanyike kama itakavyoamuliwa na Kamati ya Utendaji Mkoa kwa kipindi kisichozidi siku tisini (90).

SURA YA TANO

VIKAO VYA CHAMA

5.1 Ngazi za Vikao vya Chama.

5.1.1 Chama kitakuwa na vikao katika ngazi zifuatazo:

i) Matawi

ii) Halmashauri

iii) Mkoa

iv) Taifa

5.1.2 Vikao hivi vitafanyika kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Vikao za Chama

5.2 Vikao vya Tawi

5.2.1 Kikao cha mwanzo katika Chama kitakuwa ni kikao cha Tawi litakaloanzishwa katika mahali pa kazi penye wanachana kumi au zaidi walioajiriwa, na kuandikishwa Wizara husika.

5.2.2 Mahala pa kazi penye wanachama wasiofika kumi, shughuli zao zitaratibiwa na tawi lililo karibu

5.2.3 Katika kutekeleza majukumu yake, kutakuwa na vikao vifuatavyo katika Tawi;

i) Mkutano wa Wanachama wote

ii) Mkutano wa Wafanyakazi wote

iii) Halmashauri Kuu ya Tawi

iv) Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi.

5.3 Mkutano wa Wanachama wote

Kutakuwa na Mkutano wa Wanachama wote wa TALGWU kwa kila Tawi ambao utafanya vikao vyake vya kawaida mara moja kila baada ya miezi sita, lakini Mkutano wa wanachama wote unaweza kuitishwa kwa dharura kwa uamuzi wa Halmshauri kuu ya Tawi au kwa kuagizwa na ngazi za juu.

5.3.1 Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi, utakuwa na wajumbe wafuatao;

(i) Mwenyekiti wa Tawi

(ii) Katibu wa Tawi

(iii) Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Tawi

(iv) Wajumbe wote wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi

(v) Mwakilishi wa Tawi kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa

(vi) Viongozi wa Ngazi ya Mkoa na Taifa wanaofanya kazi katika Tawi hilo.

(vii) Wanachama wote wa Chama katika Tawi hilo

(viii) Mjumbe mwakilishi wa Wafanyakazi vijana.

(ix) Mjumbe mwakilishi wa watu wenye Ulemavu.

5.3.2 Kazi za Mkutano wa Wanachama wote

Kazi za Mkutano wa Wanachama wote wa Chama katika Tawi zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya Tawi na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa kipindi kijacho.

(b) Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi za juu yanatekelezwa ipasavyo.

(c) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi kama yatakavyowasilishwa na Halmashauri ya Tawi na kutoa maelekezo kwa kipindi kijacho.

(d) Unapofika wakati wa uchaguzi, Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi, utashughulikia mambo yafuatayo:

(i) Kuchagua Mwenyekiti wa Tawi

(ii) Kuchagua Katibu wa Tawi

(iii) Kuchagua wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi

(iv) Kuchagua Mwakilishi mmoja wa Tawi kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(v) Kuchagua wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi.

(vi) Kuchagua mjumbe mmoja mwakilishi wa watu wenye ulemavu.

(vii) Kuchagua mjumbe mmoja mwakili wa vijana kwenye Halmashauri ya Tawi.

5.4 Mkutano wa Wafanyakazi wote

Mkutano wa Wafanyakazi wote katika Tawi utafanyika mara moja kwa mwaka, lakini vikao vya dharura vinaweza kufanyika kwa kuitishwa na Mkutano wa Wanachama wote.

5.4.1 Mkutano wa wafanyakazi wote wa Tawi utakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Tawi

(ii) Katibu wa Tawi

(iii) Viongozi wote wa Chama wa ngazi za juu wanaofanya kazi kwenye Tawi hilo.

(iv) Wanachama wote wa Chama wa Tawi hilo.

(v) Wafanyakazi wote waliopo mahali hapo pa kazi.

5.4.2 Kazi za Mkutano wa Wafanyakazi wote

Mkutano wa Wafanyakazi wote katika Tawi utafanya kazi zifuatazo:

(i) Utajadili utekelezaji mzuri wa mpango wa kazi kama utakavyowasilishwa na Halmashauri Kuu ya Tawi.

(ii) Kujadili na kuhamasisha utendaji bora wa kazi mahala pa kazi.

5.5. Halmashauri Kuu ya Tawi

Kutakuwa na Halmashauri Kuu ya Tawi ambayo itafanya vikao vyake mara nne kwa mwaka na idadi ya wajumbe wake itategemea ukubwa wa Tawi husika.

5.5.1 Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi

Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi watakuwa kama ifuatavyo:

(i) Wajumbe watano akiwemo Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kama Tawi lina wanachama kumi lakini halizi wanachama hamsini.

(ii) Wajumbe kumi ambao ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kama Tawi linazidi wanachama hamsini lakini chini ya mia moja.

(iii) Wajumbe kumi na tano ambao ni pamoja na Mwenyekti na Katibeu wa Tawi kama Tawi lina wanachama wanaozidi mia moja lakini chini ya mia tano.

(iv) Wajumbe ishirini ambao ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kama Tawi lina wanachama wanaozidi mia tano lakini chini ya elfu moja.

(v) Wajumbe wa vikao vya juu vya Chama waliomo katika Tawi hilo.

(vi) Mwenyekiti na Katibu Kamati ya ushauri ya Wafanyakazi Wanawake.

(vii) Mwakilishi wa vijana na mwakilishi wa watu wenye ulemavu.

5.5.2 Kazi za Halmashauri ya Tawi

Halmashauri ya Tawi itafanya kazi zifuatazo:

(i) Kuhakikisha kuwa haki na usalama vinadumishwa mahali pa kazi.

(ii) Kufunga mikataba ya hari na kutoa taarifa ngazi za juu za Chama.

(iii) Kutoa taarifa ngazi za juu za Chama kuhusu suala lolote ambalo linaweza kusababisha Mgogoro wa Kikazi kati ya wanachama na mwajiri.

(iv) Kubuni njia za kukuza tija na kuendeleza uzalishaji na ajira ya hakika na kuhakikisha kuwa wanachama wanafaidika kutokana na ziada inayotokana na ongezeko la tija.

(v) Kutoa taarifa mara kwa mara kwa wanachama kuhusu shughuli za jumla za Tawi.

(vi) Kusajili wanachama wapya.

(vii) Kuendeleza uhusiano na matawi mengine hasa matawi yanayokuwa katika kazi za aina moja.

(viii) Kusimamia elimu ya wafanyakazi tawini.

(ix) Katika matawi makubwa, Halmashauri itachagua wawakilishi wenye kazi maalum ya kuwasiliana na wanachama katika idara au sehemu mbalimbali za mahali pa kazi.

(x) Kupanga na kutoa misaada na ushauri kwa wanachama.

(xi) Kutunza daftari la kumbukumbu za wanachama.

(xii) Kusimamia makato yatokanayo na mishahara ya wafanyakazi.

(xiii) Kuitisha Mkutano wa wanachama wote ili kupata maoni kwa njia ya kura kuhusu uwezekano wa kuitisha mgomo ikiwa mgogoro wa kikazi umeshindikana kupatiwa ufumbuzi.

(xiv) Kutangaza mgomo baada ya Wanachama kupiga kura ya maoni na zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa kuunga mkono mgomo, na uamuzi huo kuwasilishwa mbele ya Halmashauri Kuu ya Tawi ili itoe kibali baada ya kushauriana na ngazi za juu za Chama.

5.6 Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi

Kutakuwa na Kamati ya Ushauri ya wafanyakazi wanawake ya Tawi katika kila Tawi la Chama ambayo itafanya vikao vyake vya kawaida mara nne kwa mwaka lakini inaweza ikaitishwa kwa dharura pale itakapobidi.

5.6.1 Wajumbe wa Kamati ya ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi

Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi.

(ii) Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi.

(iii) Mweka Hazina wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi.

(iv) Wajumbe wawili wa kamati waliochaguliwa na Mkutano wa wanachama wote wa Tawi.

(v) Viongozi wa ngazi za juu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ambao wanafanya kazi mahali hapo pa kazi.

5.6.2 Kazi za Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi

Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Tawi itakuwa na kazi zifuatazo:

(i) Kuhamasisha wafanyakazi wanawake mahali pa kazi ili waelewe umuhimu wa Chama cha Wafanyakazi na hatimaye washiriki katika uongozi wa aina zote nchini.

(ii) Kuwa kiungo, kushauri na kupendekeza kwa Halmashauri ya Tawi masuala yote yanayohusu wafanyakazi wanawake mahali pa kazi.

(iii) Kuwaelemisha wafanyakazi walio katika Makundi Maalumu kuondokana na unyonge wa kutojiamini ili wajue kuwa wao ni sehemu ya Taifa na hakuna mipaka katika kupigania haki, usawa na kushiriki kwa ukamilifu katika kuleta maendeleo ya kijamii mahala pa kazi.

(iv) Kuwaelimisha na kuwashauri kuhusu masuala ya kiuchumi mahala pa kazi na kuwahamasisha kuanzisha Vyama vya kuweka na kukopa pamoja na miradi mingine ya kiuchumi ili kujiongezea kipato katika maisha yao ya kazi kwa lengo la kuondokana na umasikini.

(v) Kuwaelimisha kuhusu masuala ya kijamii, kijinsia na kiutamaduni pamoja na elimu ya wafanyakazi, makundi maalum katika sehemu nyingine.

(vi) Kushauri vyombo vya Chama na Taasisi nyingine za maendeleo kitaifa, masuala yote yanayohusu wafanyakazi wanawake mahali pa kazi.

5.7 Viongozi wa Chama katika Tawi

Kutakuwa na viongozi wafuatao katika kila Tawi.

(i) Mwenyekiti wa Tawi

(ii) Katibu wa Tawi

5.7.1 Mwenyekiti wa Tawi

Mwenyekiti wa Tawi atachaguliwa na Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi. Atakuwa katika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika. Katika Mkutano anayoongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa Tawi, atakuwa pia na kura ya uamuzi, endapo kura za wajumbe wanaofiki na wasioafiki zitalingana.

5.7.2 Kazi za Mwenyekiti wa Tawi

(i) Atakuwa na madaraka ya kusimamia mambo yote ya Chama katika Tawi.

(ii) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa Wanachama wote. Mkutano wa Wafanyakazi wote na Vikao vya Halmashauri Kuu ya Tawi. Kama hayupo katika kikao chochote kile, wajumbe waliopo wanaweza kuchagua mjumbe mwingine yeyote kutoka miongoni mwao kuongoza kikao hicho.

5.7.3 Katibu wa Tawi

Katibu wa Tawi atachaguliwa na Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi lake. Atakuwa katika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

5.7.4 Kazi za Katibu wa Tawi

(i) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Chama katika Tawi na atafanya kazi chini ya uongozi wa Halmashauri Kuu ya Tawi lake.

(ii) Atakuwa ndiye Mkuu wa Mipango na mfuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Chama katika Tawi lake.

(iii) Atakuwa na wajibu wa kuandaa na kuitisha vikao vya Tawi kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Tawi.

(iv) Atakuwa ndiye Afisa Masuhuli wa Chama katika Tawi.

5.8 VIKAO VYA CHAMA KATIKA HALMASHAURI

5.8.1 Kamati ya Uratibu

Kutakuwa na Kamati ya Uratibu katika kila Halmashauri ambayo itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi sita.

5.8.2 Wajumbe wa Kamati ya Uratibu

Kamati hiyo itajumuisha viongozi wafuatao katika Chama:

(i) Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa Wenyeviti wa Matawi.

(ii) Katibu atakayechaguliwa miongoni mwa Makatibu wa Matawi.

(iii) Wenyeviti na Makatibu wa Chama wa Matawi.

(iv) Viongozi wa ngazi za juu walioko katika Halmashauri hiyo.

(v) Mwakilishi mmoja wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake.

(vi) Mwakilishi wa Vijana na mwakiishi wa watu wenye Ulemavu.

5.8.3 Kazi za Kamati ya Uratibu

(i) Kujadili kwa undani kazi za Chama katika matawi.

(ii) Kubuni na kutafuta mbinu za uimarishaji wa Chama.

(iii) Kupokea na kujadili utekelezaji wa maagizo toka ngazi za juu za Chama.

(iv) Kuhakikisha utekelezaji wa maelekezo ya ngazi za juu unafanyika ipasavyo katika kila Tawi katika Halmashauri.

(v) Kupokea na kujadili taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Matawi.

(vi) Kupokea na kutunza hati za malipo na kuziwasilisha katika ngazi ya Mkoa.

5.9 VIKAO VYA CHAMA KATIKA MKOA

Chama kitakuwa na vikao vifuatavyo katika Mkoa;

(i) Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(ii) Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(iii) Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.

(iv) Mkutano Mkuu Maalumu wa Kazi wa Mkoa lbaada ya miaka miwili na nusu.

5.10 MKUTANO MKUU WA MKOA

Mkutano Mkuu wa Mkoa ndicho chombo kikuu cha Chama katika mkoa na utafanya mikutano yake mara mbili katika miaka mitano, mikutano Maalumu yaweza kuitishwa kwa idhini ya Kamati ya Utendaji ya mkoa au kwa kuagizwa na ngazi za juu za Chama.

5.10.1 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa

Mkutano Mkuu wa Mkoa utakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Mkoa.

(ii) Mjumbe wa Baraza Kuu Taifa aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(iii) Mjumbe wa Kamati ya utendaji Taifa aliyechaguliwa na mkutano Mkuu wa Mkoa.

(iv) Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(v) Wajumbe watatu wa Mkutano Mkuu wa Taifa waliochaguliwa na Mkutano mkuu wa Mkoa.

(vi) Wenyeviti wote wa Matawi yaliyomo katika Mkoa.

(vii) Makatibu wote wa matawi yaliyomo katika Mkoa.

(viii) Mwakilishi mmoja wa kila tawi lililopo katika Mkoa.

(ix) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.

(x) Wajumbe wote Kamati ya ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.

(xi) Viongozi wa ngazi za juu za Chama wanaofanya kazi katika mkoa huo.

(xii) Mwakilishi wa watu wenye ulemavu aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(xiii) Mwakilishi wa Vijana aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

5.10.2 Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa

Mkutano Mkuu wa Mkoa utafanya kazi zifuatazo:

i) Kupokea na kujadili taarifa ya shughuli za Chama na fedha itakayowasilishwa na Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

ii) Kutekeleza Maazimio yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama, Baraza Kuu la Chama na Kamati ya Utendaji ya Chama.

iii) Kuratibu na kusaidia utekelezaji wa shghuli za Chama katika Mkoa.

iv) Kujadili na kukuza hali nzuri ya maisha ya wanachama katika Mkoa.

v) Inapofika wakati wa uchaguzi Mkutano Mkuu wa Mkoa, utafanya kazi zifuatazo:

(a) Utachagua Mwenyekiti wa Mkoa.

(b) Utachagua Mjumbe wa Baraza Kuu la Taifa atayewakilisha Mkoa.

(c) Utachagua Mjumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa atakayewakilisha mkoa husika.

(d) Utachagua wajumbe watatu watakaowakilisha Mkoa katika mkutano Mkuu wa Taifa kwa kuzingatia jinsia.

(e) Utachagua wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa, mmoja toka kila Halmashauri, Shirika la Maendeleo lililopo mkoani na Mfuko wa Pensheni wa LAPF.

(f) Utachagua viongozi wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa wakiwemo Mwenyekiti, Katibu na Mjumbe mmoja mmoja toka kila Halmashauri, Shirika la Maendeleo ililopo mkoani na Mwakilishi wa Mfuko wa Pensheni wa LAPF.

(g) Utachagua mjumbe mmoja mwakilishi wa watu wenye ulemavu kuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji Mkoa.

(h) Utachagua mjumbe mmoja mwakilishi wa vijana kuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji Mkoa.

5.11 KAMATI YA UTENDAJI YA MKOA

Kutakuwa na kamati ya Utendaji ya Mkoa itakayokutana mara moja kila baada ya miezi mitatu.

5.11.1 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa

Kamati ya Utendaji wa Mkoa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Mkoa.

(ii) Mjumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(iii) Mjumbe wa Baraza Kuu la Taifa aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(iv) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa, Mwakilishi mmoja mmoja toka kila Halmashauri, Shirika la Uchumi la Halmashauri na Mjumbe mmoja toka mfuko wa Pensheni wa LAPF.

(v) Wajumbe watatu wa Mkutano Mkuu wa Taifa waliochaguliwa na Mkutano wa Mkoa.

(vi) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.

(vii) Viongozi wa ngazi ya Taifa wanaofanya kazi katika mkoa huo.

(viii) Mjumbe mmoja mwakilishi wa watu wenye ulemavu aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa mkoa.

(ix) Mjumbe mmoja mwakilishi wa vijana aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

5.11.2 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Mkoa

Kamati ya Utendaji ya mkoa itafanya kazi zifuatazo:

(i) Kutekeleza maazimio ya vyombo vya juu vya Chama.

(ii) Kuratibu na kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za Chama.

(iii) Kusaidia Matawi na kamati za Uratibu za Halmashauri katika shughuli mbalimbali za Chama.

(iv) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi na fedha iliyotolewa na Katibu wa Mkoa.

(v) Kuanzisha matawi mapya sehemu za kazi katika mkoa husika.

(vi) Kusimamia nidhamu kwa watumishi wa mkoa na viongozi wa matawi.

(vii) Kupokea na kujadili taarifa za mapato na matumizi ya fedha za Chama katika matawi zilizowasilishwa na Waratibu.

(viii) Kujaza nafasi za viongozi zilizo wazi katika mkoa husika.

5.12 Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.

Kutakuwa na Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa ambayo itafanya Vikao vyake mara nne kwa mwaka.

5.12.1 Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.

Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya mkoa.
(ii) Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.
(iii) Mweka Hazina wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Mkoa.
(iv) Mjumbe mmoja mmoja toka kila Halmashauri, Shirika la Maendeleo na Mfuko wa Pensheni wa LAPF.
(v) Viongozi wa ngazi za juu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ambaye anafanya kazi katika Mkoa huo.

5.12.2 Kazi za Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya mkoa.

(i) Itaandaa mpango wa kuhamasisha wafanyakazi wanawake mkoani katika kuelewa umuhimu wa Chama cha Wafanyakazi na kuhamasisha ushirikishwaji katika uongozi wa Chama, Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za umma Nchini.

(ii) Kuwa kiungo, kushauri na kupendekeza kwa Kamati ya Utendaji ya Mkoa, masuala yote yanayohusu wafanyakazi wanawake katika mkoa husika kabla ya kushughulikiwa kisheria na Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(iii) Kujizatiti kutoa maelekezo katika kuwaelimisha wafanyakazi wanawake ili wapate kujikwamua katika unyonge wa kutojiamini na kujua kuwa wao ni sehemu ya Taifa katika kupigania haki, usawa na kushiriki kwa ukamilifu katika kuleta maendeleo ya jamii mahala pao pa kazi na katika sehemu nyingine katika Taifa letu.

(iv) Kuwaelimisha na kuwahamisha wafanyakazi kuhusu masuala ya kiuchumi mahala pa kazi kwa kuwashauri kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa ili kujiongezea vipato katika maisha yao na kuondokana na umaskini mahala pa kazi.

(v) Kuwaelimisha wafanyakazi wanawake masuala ya kijinsia na kiutamaduni ikiwemo elimu ya wafanyakazi kuhusu sheria, nidhamu, kanuni za utii katika kazi na uzoefu wa wafanyakazi wanawake katika Nchi zingine.

(vi) Kuwa chombo cha kushauri Chama na Taasisi nyingine za maendeleo kitaifa katika masuala yote yanayohusu wafanyakazi wanawake mahala pao pa kazi na katika kupigana haki zao.

5.13 VIONGOZI WA CHAMA WA MKOA

Kutakuwa na Viongozi wafuatao katika mikoa;

(i) Mwenyekiti wa Mkoa

(ii) Katibu wa Mkoa

5.13.1 Mwenyekiti wa Mkoa

(i) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa na atashika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(ii) Katika mikutano anayoingoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa Mkoa atakuwa pia na kura ya uamuzi iwapo kura za wanaoafiki na wasioafiki zitalingana.

5.13.2 Kazi za Mwenyekiti wa Mkoa

(i) Atakuwa na madaraka ya kusimamia mambo yote ya Chama katika Mkoa.

(ii) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Mkoa na Kamati ya Utendaji ya Mkoa. Kama hayupo katika kikao chochote kile, wajumbe waliopo watachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao husika.

(iii) Atatia saini katika kumbukumbu akishirikiana na katibu wa Mkoa.

(iv) Atashauriana na Katibu wa Mkoa kupanga vikao vya Mkoa.

5.13.3 Katibu wa Mkoa

Ataajiriwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Taifa baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama. Atawajibika kwa Katibu Mkuu kuhusu mwenendo wa shughuli zote za Chama mkoani kwake.

5.13.4 Kazi za Katibu wa Mkoa

(i) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Chama mkoani kwake na atafanya kazi chini ya uongozi wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(ii) Atasimamia Kamati za Uratibu za Wilaya na Makatibu wa Matawi ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi katika Mkoa wake ni wanachama na fedha za Chama zinatumika ipasavyo.

(iii) Atakuwa ndiye Katibu wa Vikao vyote vya Chama katika Mkoa.

(iv) Atatisha vikao vyote vya mkoa akishirikiana na Mwenyekiti wa mkoa kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

(v) Atakuwa Afisa Masuhuli wa Fedha za Chama katika Mkoa.

(vi) Atatia saini katika Hundi zote za Chama na kuwajibika kufanya mawasiliano yote yanayohusika.

(vii) Atatunza vitabu na hati za malipo na kuwasilisha taarifa ngazi ya Taifa.

(viii) Atakuwa ndiye Msemaji Mkuu wa Chama kwa masuala yote yanayohusu shughuli za Chama katika ngazi ya Mkoa.

(ix) Atawasilisha taarifa ya fedha ya kila robo (1/4) mwaka na ya mwaka mzima kwa Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(x) Atawasilisha kwa Katibu Mkuu taarifa za kazi za Chama zilizopitishwa na vikao vinavyohusika mkoani kwake kila robo mwaka, na ya mwaka mzima.

5.14 VIKAO VYA TALGWU TAIFA

Kutakuwa na Vikao vya Chama vifuatavyo katika ngazi ya Taifa:

(i) Mkutano Mkuu wa Taifa.

(ii) Baraza Kuu la Taifa.

(iii) Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(iv) Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa.

(v) Mkutano Mkuu Maalum wa Kazi baada ya miaka miweili na nusu.

(vi) Kikao cha Tathmini cha Wenyeviti wa mikoa mara moja kwa mwaka.

5.15.1 MKUTANO MKUU WA TAIFA

Mkutano Mkuu wa Taifa ndicho chombo kikuu cha Chama na utafanya mikutano yake mara mbili katika kipindi cha miaka mitano (5). Mikutano Maalum inaweza kuitishwa na Baraza Kuu la Taifa kwa

uamuzi wa theluthi mbili ya wajumbe wa Baraza Kuu. Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Chama itatolewa miezi mitatu kabla ya kikao husika, vinginevyo taarifa ya muda mfupi itatolewa kama itabidi kuitisha mkutano Maalum.

5.15.2 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:

(ii) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.

(ii) Makamu wa Mwenyekiti wa Chama.

(iii) Katibu Mkuu wa Chama

(iv) Naibu Katibu Mkuu wa Chama.

(v) Mweka Hazina wa Chama.

(vi) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(vii) Wenyeviti wote wa Mikoa.

(viii) Wadhamini wa Chama.

(ix) Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho toka TALGWU.

(x) Wajumbe wa Baraza Kuu la Chama.

(xi) Wawakilishi watatu (3) kutoka kila Mkoa watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(xii) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa.

(xiii) Wajumbe wote wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa.

(xiv) Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho toka TALGWU.

5.15.3 Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utafanya kazi zifuatazo:

(i) Utapokea toka Baraza Kuu la Taifa taarifa ya Kazi za chama kwa kipindi husika na kuzichambua na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa kipindi kinachofuata.

(ii) Kuthibitisha kubadili, kukataa au kuvunja maamuzi yoyote yaliyotolewa na Kikao chochote cha chini yake au Mkuu yeyote wa Chama.

(iii) Kubadili sehemu yoyote ya Katiba ya Chama kwa uamuzi wa theluthi mbili ya wajumbe wenye haki ya kupiga kura.

(iv) Kuthibitisha Sera kulingana na wakati na mahitaji ya Chama, zikiwemo zile zinazohusu uamuzi kuhusu shughuli za uhusiano wa Kimataifa na kuhusu Chama kujiunga na Taasisi za Vyama vya Kitaifa na Kimataifa kama itakavyopendekezwa na Baraza Kuu.

(v) **Inapofika wakati wa uchaguzi, Mkutano Mkuu wa taifa utafanyaka kazi zifuatazo:**

(a) Utachagua Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.

(b) Utachagua Makamu Mwenyekti wa Chama.

(c) Utachagua Katibu Mkuu wa Chama.

(d) Utachagua Mwenyekiti wa Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Taifa.

(e) Utachagua Wawakilishi wa Chama katika Mkutano Mkuu wa Shiriisho.

5.16.1 BARAZA KUU LA TAIFA

Kutakuwa na Baraza Kuu la Taifa ambalo litafanya vikao vyake vya kawaida mara moja kwa mwaka isipokuwa vikao maalum vinaweza kuitishwa kwa uamuzi wa Kamati ya Utendaji ya Taifa. Baraza Kuu litakutana mara moja kwa mwaka kabla ya mwisho wa mwezi wa kwanza (Januari) na taarifa ya kikao itatolewa katika kipindi kisichopungua mwezi mmoja kabla ya kikao husika.

5.16.2 Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa

Wajumbe wa Baraza Kuu watakuwa wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.
(ii) Makamu wa Mwenyekiti wa Chama.
(iii) Katibu Mkuu wa Chama.
(iv) Naibu Katibu Mkuu wa Chama
(v) Mweka Hazina wa Chama.
(vi) Wenyeviti wote wa Mikoa.
(vii) Mjumbe mmoja kutoka kila Mkoa.
(viii) Wajumbe Kamati ya Utendaji ya Taifa.
(ix) Wajumbe kumi na nne wa Baraza Kuu la Shirikisho.
(x) Mjumbe mmoja anayewakilisha Chama kwenye Kamati ya Utendaji ya Shirikisho.
(xi) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa.
(xii) Wadhamini wa Chama.

5.16.3 Kazi za Baraza Kuu la Taifa.

Baraza Kuu la Taifa litafanya kazi zifuatazo:

(i) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za Chama na taarifa ya fedha za Chama kama itakavyowasilishwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(ii) Kuthititisha na kuhakikisha kwamba shughuli za Kamati ya Utendaji na Taifa zinaendeshwa kwa Mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

(iii) Kuthibitisha Viwango vya Posho na Mishahara kwa Viongozi, Maafisa na Watendaji wote wa Chama.

(iv) Kupokea na kujadili Mapendekezo ya kuwathibitisha Maafisa na Watendaji walioajiriwa kama itakavyowasilishwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(v) Baraza Kuu litaamua uanzishaji wa Mikoa na Halmashauri mpya.

(vi) Kupokea na kujadili Taarifa ya Mapato na matumizi ya fedha za Chama kwa mwaka unaomalizika.

(vii) Kupokea, kujadili na kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya fedha za Chama kwa mwaka unaofuata.

(viii) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Taifa.

(ix) Kuwa chombo cha Rufaa kwa vikao vyote vya chini yake.

(x) Kupokea, kujadili na kuthibitisha Kanuni zote za Chama.

(xi) **Inapofika wakati wa uchaguzi, Baraza Kuu la Taifa, litafanya kazi zifuatazo:**

(a) Kuchagua Naibu Katibu Mkuu wa Chama.

(b) Kuchagua Mweka Hazina wa Chama.

(c) Kuchagua wajumbe kumi na nne wa kuingia kwenye Baraza Kuu la Shirikisho kwa kuzingatia Jinsia.

(d) Kuchagua mjumbe mmoja kuingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Shirikisho.

(e) Kuchaga Wadhamini wa Chama.

(f) Kuchagua mjumbe mmoja mwakilishi wa watu wenye ulemavu akakayechaguliwa miongoni mwa wawakilishi wa Mikoa kuingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(g) Kuchagua mjumbe mmoja mwakilishi wa wafanyakazi vijana atakayechaguliwa miongoni mwa wawakilishi wa mikoa kuingia kwenye Kamati ya Utendaji Taifa.

(h) Kuchagua mjumbe mwakilishi wa mfuko wa Pensheni wa LAPF na mjumbe mwakilishi wa mashirika ya Uchumi kuingia Kamati ya Utendaji Taifa.

(i) Kwa idhini ya Mkutano Mkuu na bila kuathiri Katiba hii, Baraza Kuu litafanya uchaguzi ili kujaza nafasi wazi za Taifa

isipokuwa nafasi ya Mwenyekiti wa Chama wa Taifa, Makamu Mwenyekiti wa Chama na Katibu Mkuu wa Chama.

5.17.1 KAMATI YA UTENDAJI YA TAIFA

Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa ambayo itafanya vikao vyake vya kawaida mara nne kwa mwaka. Isipokuwa vikao maalum vinaweza kuitishwa na Sekretarieti ama kuagizwa na Baraza Kuu la Taifa.

5.17.2 Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa

Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao;

(i) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.
(ii) Makamu Mwenyekiti wa Chama.
(iii) Katibu Mkuu wa Chama.
(iv) Naibu Katibu Mkuu wa Chama.
(v) Mweka Hazina wa Chama.
(vi) Mjumbe mmoja wa Kamati ya Utendaji ya Taifa kutoka kila Mkoa.
(vii) Mjumbe mmoja mwakilishi wa wafanyakazi wa Mashirika ya Uchumi ya Halmashauri.
(viii) Mjumbe mmoja mwakilishi wa Wafanyakazi wa Mfuko wa Penseni wa LAPF.
(ix) Wajumbe wawili wa kuteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa.
(x) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa.

(xi) Mjumbe mmoja Mwakilishi wa watu wenye Ulemavu Taifa.

(xii) Mjumbe mmoja mwakilishi wa waanyakazi Vijana Taifa.

5.17.3 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Taifa

Kamati ya Utendaji ya Taifa itafanya kazi zifuatazo:

(i) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za Chama za kila siku.

(ii) Kupendekeza taratibu za michango na kuweka viwango.

(iii) Kupendekeza Kanuni mbalimbali za Chama.

(iv) Kuwa Mamlaka ya Nidhamu kwa watendaji na watumishi wote wa Chama walioajiriwa na kikao hicho ama Mamlaka zilizochini yake.

(v) Kuajiri watendaji wote wa Chama isipokuwa wale wa kuchaguliwa.

(vi) Kuandaa Agenda za Baraza Kuu la Taifa.

(vii) Kubuni Sera za kutoa motisha kwa watumishi wa Chama.

(viii) Kutunga Kanuni za fedha na mali za Chama.

(ix) Kubuni sera za kutoa motisha kwa wanachama kila inapowezekana.

(x) Kuwa chombo cha rufaa kwa Watumishi walio katika mamlaka ya nidhamu ya Katibu Mkuu.

(xi) Kupendekeza kwenye Baraza Kuu la Taifa hitaji la Chama, kukopa katika benki na Taasisi mbalimbali.

(xii) Kupendekeza kwenye Baraza kuu la Taifa fedha za Chama kuwekezwa katika maeneo mbalimbali ya Uwekezaji kama vile majengo na vitega Uchumi vingine vinavyoweza kuongeza mapato kwa Chama.

(xiii) Kupendekeza kwenye Baraza Kuu la Taifa Mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi maalum (Specia Audit) wa fedha na mali za Chama itakapohitajika.

(xiv) Inapofika wakati wa uchaguzi, Kamati ya Utendaji ya Taifa itafanya kazi zifuatazo:

(a) Kuratibu majina ya wanaoomba uongozi na kuyafikisha kwenye kikao cha Baraza Kuu kwa Uchaguzi ama hatua zaidi.

(b) Kupendekeza majina ya wanachama kwa taasisi zinazohitaji wawakilishi kutoka TALGWU.

5.18.1 Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake ya Taifa

Kutakuwa na Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa ambayo itakutana mara moja kwa mwaka.

5.18.2 Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa

(a) Mwenyekiti wa Kamati.

(b) Katibu wa Kamati.

(c) Mweka Hazina wa Kamati.

(d) Mjumbe mmoja mwakilishi wa wafanyakazi wanawake wa Halmashauri za Jiji.

(e) Mjumbe mmoja mwakilishi wa Mashirika ya Uchumi ya Halmashuri.

(f) Mjumbe mmoja mwakilishi wa wafanyakazi wanawake toka Halmashauri za Miji.

(g) Mjumbe mmoja mwakilishi wa wafanyakazi wanawake toka Halmashauri za manispaa.

(h) Wajumbe watatu (3) wawakilishi wa wafanyakazi Wanawake toka Halmashauri za Wilaya.

5.18.3 Kazi za Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa.

Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake itafanya kazi zifuatazo;

(i) Itaandaa mpango wa kuhamasisha wafanyaazi Wanawake kitaifa katika kuelewa umuhimu wa Vyama vya Wafanyakazi na kuhamasisha ushikishwaji katika uongozi wa Vyama, Serikalini na Taasisi nyingine za Umma Nchini.

(ii) Itakuwa ni kiungo cha kushauri na kupendekeza kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa, Baraza Kuu na Mkutano Mkuu wa Chama masuala yote yanayohusu wafanyakazi wanawake katika Serikali za Mitaa Nchini kabla ya kushughulikiwa kisheria na vikao vya kikatiba vya Chama.

(iii) Itaandaa utaratibu wa namna ya kuwaelimisha wafanyakazi wanawake katika serikali za mitaa na kutoa ushauri kwa Chama katika kubuni sera ya wafanyakazi wanawake katika

kuondokana na unyonge wa kutojiamini ili wajione wao ni sehemu ya Taifa katika kupigania haki, usawa katika kuleta maendeleo ya jamii mahali pa kazi na katika sehemu nyingine za Taifa letu.

(iv) Kuandaa na kuwahamasisha wafanyakazi wanawake mahala pa kazi katika masuala ya uchumi na kuwashauri katika kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa na miradi mingine ya kiuchumi kwa wafanyakazi wanawake ili kujiongezea vipato.

(v) kubuni sera na mikakati inayowezesha kupata marafiki katika Nchi nyingine duniani kama zipo zenye mwelekeo wa aina inayofanana na shughuli za Kamati yetu ya wafanyakazi wanawake kitaifa katika maisha yao ya kazi katika mpango wa Taifa wa kupambana na umaskini.

(vi). Kuwaelimisha wafanyakazi masuala ya kijinsia na utamaduni, pamoja na kuhimiza elimu ya sheria za kazi, nidhamu, kanuni za utii katika kazi, pamoja na kuangalia uzoefu wa wafanyakazi wanawake katika Nchi nyingine duniani.

(vii). Kuwa chombo cha kuukishauri Chama kuhusu masuala ya jumla ya wafanyakazi wanawake katika Serikali za Mitaa Nchini ikiwemo misingi ya kupigania haki na maslahi yao.

5.19 VIONGOZI WA CHAMA WA TAIFA

Katika ngazi ya Taifa, Chama kitakuwa na viongozi wakuu wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.
(ii) Makamu Mwenyekiti wa Chama.

(iii) Katibu Mkuu wa Chama.

(iv) Naibu Katibu Mkuu wa Chama.

(v) Mweka Hazina wa Chama.

5.19.1 Mwenyekiti wa Chama wa Taifa

(i) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa ndiye Kiongozi Mkuu wa Chama na atasimamia shughuli na taratibu zote za Chama.

(ii) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na atakuwa katika nafasi hiyo ya Uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(iii) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, Baraza Kuu la Taifa na Kamati ya Utendaji ya Taifa. Katika Mikutano anayoiongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, atakuwa pia na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana.

(iv) Iwapo Mwenyekiti na Makamu wake hawapo, mjumbe yeyote atachaguliwa na wajumbe kuwa mwenyekiti wa kikao hicho.

(v) Atatia saini katika kumbukumbu za Mikutano akishirikiana na Katibu Mkuu wa Chama.

5.19.2 Makamu Mwenyekiti wa Chama.

(i) Kutakuwa na Makamu Mwenyekiti wa Taifa atakayechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

(ii) Makamu Mwenyekiti wa Taifa atakuwa katika madaraka hayo kwa muda wa miaka mitano lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(iii) Makamu Mwenyekiti atakuwa ndiye msaidizi mkuu wa Mwenyekiti wa Taifa na atafanya kazi zote atakazopewa na mwenyekiti wa Taifa.

(iv) Atakuwa Mwenyekiti wa Vikao vyote vya Taifa iwapo Mwenyekiti hatokuwepo.

(vi) Inapotokea Mwenyekiti wa Chama hayupo au kiti chake kipo wazi kwa sababu yoyote ile, Makamu Mwenyekiti atakuwa na mamlaka yote ya Mwenyekiti wa Chama hadi hapo vikao vya Chama vyenye mamlaka vitakapoamua vinginevyo.

5.19.3 Katibu Mkuu wa Chama

Kutakuwa na Katibu Mkuu wa Chama atakayechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na atakaa katika madaraka hayo kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

5.19.4 Kazi za Katibu Mkuu wa Chama

(i) Atakuwa Katibu wa Mkutano Mkuu wa Taifa , Baraza Kuu la Taifa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(ii) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Chama na ataafanya kazi chini ya uongozi wa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(iii) Atakuwa ndiye Msemaji mkuu wa Chama

(iv) Atakuwa Afisa Masuhuli wa Chama na atawajibika kwa Chama kuhusu fedha za Chama.

(v) Ataweka kumbukumbu za Mikutano na kutekeleza Sera za Chama pamoja na maamuzi yaliyokwishapitishwa na Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji ya Taifa

(vi) Atatayarisha na kuwasilisha Taarifa ya Fedha za Chama kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa kila robo mwaka, na kwa Baraza Kuu la Taifa kila mwisho wa mwaka.

(vii) Atatia saini katika kumbukumbu za mikutano kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.

(viii) Ataitisha vikao vyote vya kitaifa kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Chama.

5.19.5 Naibu Katibu Mkuu wa Chama

(i) Kutakuwa na Naibu Katibu Mkuu wa Chama atakayechaguliwa na Baraza Kuu la Taifa.

(ii) Naibu Katibu Mkuu atakaa katika madaraka hayo kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya miaka hiyo kumalizika.

(iii) Atakuwa Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu na atafanya kazi zote za Chama kama atakavyoelekezwa na Katibu Mkuu.

(iv) Atakuwa Mhusika Mkuu kwa majukumu ya uimarishaji, uhamasishaji na Utawala.

5.19.6 Mweka Hazina wa Chama

(i) Kutakuwa na Mweka Hazina wa Chama atakayechaguliwa ama kuteuliwa na Baraza Kuu la Taifa.

(ii) Mweka Hazina wa Chama atakuwa katika madaraka hayo kwa muda wa miaka mitano lakini anaweza kuchaguliwa au kuteuliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(iii) Atakuwa ni Kiongozi wa kuchaguliwa na siyo Mwajiriwa wa Chama (Honorary Treasurer).

(iv) Atakuwa ni msimamizi katika masuala ya fedha na atabuni njia za kukipatia Chama mapato na mpango mzuri wa utunzaji wa fedha za Chama.

(v) Atawajibika kwa Katibu Mkuu na Kamati ya Utendaji Taifa

SURA YA SITA

6.0 Wadhamini wa Chama

Kutakuwa na wadhamini wanne watakaochaguliwa au kuteuliwa na Baraza Kuu la Chama kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Taifa. wadhamini wa Chama watakaa katika madaraka hayo kwa muda wa miaka mitano, lakini wanaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

6.1 Vikao vya Wadhamini

Wadhamini wa Chama watafanya vikao vyao mara mbili kwa mwaka.

6.2 Sifa za Wadhamini

Wadhamini wa Chama wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo:

(i) Wawe wanachama waadilifu na waaminifu katika sehemu zao za kazi na wenye upeo wa kuweza kuelewa na kuhoji masuala ya fedha za Chama.

(ii) Wasiwe na nafasi za uongozi katika Chama

(iii) Wawe wafanyakazi walioajiriwa

(iv) Wawe wanalipa michango yao

6.3 Kazi na Wajibu wa Wadhamini

Wadhamini watakuwa na kazi zifuatazo:

(i) Wadhamini watakua na wajibu wa kusimamia, kukagua na kutoa taarifa kwenye Baraza Kuu kuhusu hali ya mali za Chama.

(ii) Hati zote za kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika na Hati nyingine zozote za Chama zitakuwa chini ya Wadhamini, na zitakuwa zinatunzwa na Katibu Mkuu ambaye atazitoa kwa Wadhamini kila watakapozihitaji.

(iii) Uwekezaji Rasilimali za Chama utaamuliwa na Kamati ya Utendaji Taifa. Mdhamini haruhusiwi kuwekeza mali yoyote kama kitega uchumi kwa udhamini wa mali yake kinyume cha Kanuni za Chama.

6.4 Ukomo wa Udhamini

Nafasi ya Mdhamini wa Chama itatangazwa kuwa iko wazi na Kamati ya Utendaji Taifa, Mdhamini atahesabika kuwa ameondolewa katika shughuli zake iwapo mambo yafuatayo yatatokea:

(i) Atajiuzulu kwa kumwandikia barua Katibu Mkuu wa Chama

(ii) Atathibitika kuwa na ugonjwa wa akili

(iii) Atapatikana na hatia ya shitaka la jinai

(iv) Hatakuwepo sehemu yake ya kazi kwa muda unaozidi miezi sita

(v) Atastaafu kazi kwa muhibu wa Sheria

(vi) Akiacha au kuachishwa kazi.

(vii) Atafariki.

SURA YA SABA

7.0 MALI, VITEGA UCHUMI NA MIKOPO YA CHAMA

Bila kuathiri masharti ya ibara ya 1.4 ya Katiba hii, Chama kitawekeza fedha zake katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kukijengea uwezo kiuchumi ili kukiwezesha kuwa na uwezo wa kuhudumia wanachama wake ipasavyo. Katika kutekeleza lengo hili, Chama kitakuwa na uwezo wa;

i) Kuanzisha, kumiliki na kuendesha miradi mbalimbali kama itakavyopendekezwa na Kamati ya Utendaji Taifa na kuamuliwa na Baraza Kuu.

ii) Kubuni miradi ya maendeleo kama vile Majengo, Hisa katika makampuni mbalimbali, Amana za Serikali (Government Bills and Bonds), kama vyanzo mbalimbali vya mapato ya Chama.

iii) Kutafuta fedha za kuendesha miradi yake ya maendeleo kutoka katika Taasisi za fedha za nje na ndani kama vile Mabenki, watu binafsi na taasisi nyingine zinazojihusisha na masuala ya kutoa mikopo mbali na Mabenki.

SURA YA NANE

8.1 UWASILISHAJI WA HOJA

(i) Wanachama binafsi na wa matawi watakuwa na haki ya kupeleka hoja zao katika vikao vya Mkutano Mkuu wa Chama. Hoja binafsi za wanachama hata kama Mkutano Mkuu wa Tawi hauziafiki, utazipitisha na kuzipeleka Makao Makuu ya Chama ili zikajadiliwe na kufanyiwa uamuzi na vikao husika. Hoja hizo zifikishwe Makao Mkuu ya Chama miezi mitatu kabla ya Mkutano Mkuu.

(ii) Kamati ya Utendaji Taifa itajadili na kutoa uamuzi wa hoja zilizowasilishwa, na itatoa sababu ya kufikia uamuzi wake kwa Baraza Kuu la Taifa.

(iii) Baraza Kuu la Taifa litajadili na kutoa uamuzi wa hoja zilizowasilishwa, na litatoa sababu ya kufikia uamuzi wake kwa Mkutano Kuu wa Taifa.

(iv) Hoja na mapendekezo zitagawiwa kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa Maandishi katika muda unaofaa kabla ya kikao cha Mkutano Mkuu kuanza.

(v) Hoja za wanachama katika ibara hii zitajumuisha pia hoja za kuhusu kubadili sehemu au ibara yoyote ya Katiba hii.

8.2 Mapato ya Chama

(i) Chama kitaendesha shughuli zake kutokana na fedha zilizotokana na michango ya kila mwezi, misaada kutoka kwa wafadhili, wahisani, miradi ya uchumi na misaada kutoka kwa Vyama Rafiki vya Wafanyakazi, Taasisi, Watu Binafsi na fedha hizo zitatumika kwa mujibu wa Katiba hii.

(ii) Chama kitakuwa na Mfuko wa Mshikamano (Solidarity Fund) ambao uendeshwaji wake utapendekezwa na Baraza Kuu la Taifa.

8.3 Mgawanyo wa Mapato ya Chama

Utatokana na mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Taifa.

8.4 Ukaguzi wa Fedha za Chama

Hesabu za fedha za Chama zitakaguliwa mara moja kwa mwaka na mkaguzi anayekubalika au mkaguzi mahsusi aliyeteuliwa na Baraza Kuu la Chama Januari hadi Desenba kila mwaka.

8.5 Utata wa Tafsiri ya Katiba

Mgogoro wowote utakaotokana na tofauti ya tafsiri ya Katiba hii kati ya Chama, Matawi, Kamati zilizochaguliwa, Viongozi waliochaguliwa au wanachama unaweza kupelekwa kwenye Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi na hatimaye kwa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi Nchini ili kupata ufafanuzi au mwongozo.

8.6 Kuvunjika kwa Chama au Kuunganisha Vyama

(i) Kuvunjwa kwa Chama

Chama kinaweza kuacha kufanya shughuli zake au kuvunjwa kama pendekezo litapitishwa na theluthi mbili ya wanachama wote na mali na madeni yote yatakuwa chini ya Usimamizi wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini – RITA

(ii) Uamuzi wa Kuungana na Chama Kingine

Uamuzi wa kujiunga na Chama kingine unaweza kuchukuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama ukizingatia maoni yaliyowasilishwa kwa njia ya Hoja, au Mapendekezo ya Kamati ya Utendaji na kukubaliwa na Baraza Kuu la Chama. Hoja hizo na mapendekezo yake ni lazima kupigiwa kura na Mkutano Mkuu kama wajumbe wake watakuwa wamepata taarifa ya miezi mitatu kabla ya Mkutano.

8.7 Upigaji wa Kura

Wakati wowote ambapo kutahitajika kupiga kura ili kufikiwa kwa uamuzi, kura za siri zitapigwa ikiwa uamuzi huo utahusisha:

i) Uchaguzi wa viongozi wa Chama.
ii) Maoni juu ya kuridhiwa kwa mgogoro.
iii) Kubadili sehemu yoyote ya Katiba au Kanuni za Chama.
iv) Kuvunjika au kuunganika kwa Chama.
v) Suala lolote linalowaathiri Wanachama kwa kiwango kikubwa.

8.8 Migogoro ya Kikazi au Mijadala na Mwenendo

Sera ya Ujumla

1. Kamati ya Utendaji ya Taifa itawajibika kwa maazimio yanayotokana na majadiliano na migogoro lakini itakasimu madaraka yake kwa Katibu Mkuu.

2. Kwa upande wa majadiliano au Mkataba unaohusu sekta nzima ya kikazi iwapo Matawi yenye watu wengi yatahusishwa. Katika hali hiyo, Baraza la Majadiliano la Kitaifa linaweza kuanzishwa. Hata hivyo kazi ya Baraza hilo itakuwa ni kutoa ushauri zaidi na siyo kuwa chombo cha majadiliano ambacho kitawajibika kwa masuala yote ya utendaji ya Chama. Baraza la Majadiliano linaweza kuchagua mjumbe wa kushughulikia majadiliano na Chama cha Waajiri (au Mamlaka yoyote ya Umma) Baraza hili kila mara ni lazima liongozwe na Katibu Mkuu au mmoja wa wasaidizi wa sekta inayohusika.

3. Matawi yana haki ya kujitetea chini ya Mwajiri na kuendesha shughuli za majadiliano Tawini. Hata hivyo ili kuhakikisha kuwa kamati ya Utendaji ina mipango mizuri kuhusu Sera za Mishahara na maslahi mengine ya watumishi Nchini, Mikataba kwenye matawi itawasilishwa mbele ya Kamati ya Utendaji Taifa kwa uthibitisho kabla ya kutiliana sahihi.

4. Matawi yatawajibika kutoa taarifa mkoani na hatimaye Makao Makuu ya Chama ili kuirahisishia Makao Makuu ya Chama kusaidia kabla ya matatizo hayajawa makubwa.

5. Ili kuzuia migogoro isiyokuwa ya lazima kutokea ni vema kura ya maoni kuhusu mgomo ipigwe katika kikao cha wanachama wote wa Tawi na azimio la mgomo litekelezwe kwa uamuzi ya zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa na wanachama kuunga mkono mgomo ili kukidhi masharti ya kuitisha mgomo kwa mujibu wa sheria.

6. Maoni ya kura ya mgomo yatasaidia kuonyesha kuwa wengi wa wanachama watapendelea kufanya mgomo na kuongeza msukumo kwa mwajiri kukubaliana kutafuta suluhisho endapo uamuzi wa kugoma umefikiwa.

7. Kamati ya utendaji Taifa itahusika katika kuratibu migomo itakayoitishwa na Chama, na endapo Shirikisho au Chama Shiriki kitaitisha mgomo au kitendo cha kupinga na kuomba ushiriki wa Chama, Katibu Mkuu atawasilisha maombi hayo kwa Kamati ya Utendaji Taifa kwa uamuzi.

8. Kamati ya Utendaji Taifa inaweza kuanzisha Mfuko Maalum utakaolenga kukiwezesha Chama kukabiliana na athari za mgomo mkubwa ikiwa ni pamoja na kutunzia wanachama watakaoathirika kwa muda mrefu na mgomo husika.

9. Utekelezaji wa Katiba za Chama kuhusiana na migogoro au migomo kutarahisisha Shirikisho kuwa na uwezo wa kuishawishi Serikali kuacha kutunga Sheria zisizokubaliana na maslahi ya wafanyakazi.

10. Endapo patatokea mgongano wowote wa kisheria kati ibara yoyote ya Katiba hii na Sheria za nchi sheria za nchi zitatumika.